# DHIMA YA TAFSIRI HIFADHI: UCHUNGUZI WA *BIBLIA TAKATIFU*

*Rehema Stephano* na *Emanuel Samwel Kaghondi*

**Ikisiri**

*Makala hii inafafanua dhima ya tafsiri hifadhi katika Biblia. Msingi wa makala hii ni kubainisha, kuchambua na kueleza dhima ya maneno ya lugha chasili ambayo yameendelea kuwapo katika Biblia hadi sasa. Maswali yanayoongoza makala hii ni mawili. Je, maneno yapi katika Biblia ni ya lugha chasili? Kwa nini maneno hayo yaendelee kuwapo katika lugha lengwa, hasa Kiswahili? Methodolojia ya utafiti huu ni uchanganuzi wa maneno yaliyopo katika tiniwayo katika Biblia: Maandiko Matakatifu toleo la mwaka 1997. Makala inabainisha kwamba tafsiri hifadhi ina dhima kubwa, hasa katika Biblia. Aidha, matokeo ya uchambuzi wetu yanaonesha kwamba tafsiri hifadhi, pamoja na dhima nyinginezo, inatunza utukufu wa Kimungu, historia na kumbukumbu ya mambo mbalimbali na kuonesha msisitizo wa mambo ya Kimungu. Kutokana na matokeo haya, makala hii inapendekeza kwamba, wasomaji wa tafsiri hifadhi wajijuvye vya kutosha kuhusu masalia ya lugha chanzi yaliyomo katika matini lengwa, hususani Biblia, ili waweze kuelewa ujumbe uliomo katika matini husika. Wasomaji hawa wataweza kujijuvya dhima za masalio yaliyopo katika maandiko kupitia kamusi, kusoma maandiko mengine yenye welekeo moja na kuwakabili wazungumzaji wa lugha chanzi.*

## Utangulizi

Tafsiri ni uhawilishaji wa taarifa za kimaandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi - LC) kwenda katika lugha nyingine (lugha lengwa - LL). Kuna aina kuu nne za tafsiri ambazo ni tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano (Mwansoko na Wenzake, 2015). Tafsiri ya neno kwa neno ni ile ambayo kila neno pamoja na mofimu zake hufasiriwa kwa maana ya kikamusi kwa kufuatishwa chini ya matini chanzi (MC) yake. Maneno ya kitamaduni, tamathali za semi, nahau, misemo na methali hutafsiriwa kwa kutumia maana za msingi pia. Tafsiri sisisi ni ile ambayo maneno, yakiwemo yale ya kitamaduni, hutafsiriwa kwa kuzingatia maana zake za msingi, ila kwa kuzingatia sarufi ya LL. Tafsiri ya kisemantiki ni ile inayozingatia vipashio vyote vya MC na kuvifasiri kwa vipashio vyake katika LL. Tafsiri ya kimawasiliano ni ile inayozingatia maana, mtindo, muundo, mazingira na utamaduni wa LL katika kuhawilisha taarifa za MC kwenda katika matini lengwa (ML). Kwa upande mwingine, Nord (2005), kama anavyonukuliwa na Munday (2008), kupitia Nadharia ya Uchambuzi Matini ya miaka ya 1980, anabainisha aina mbili za tafsiri. Nazo ni tafsiri hifadhi na tafsiri

wenzo kama zilivyotafsiriwa na Mpemba (2016) kutoka dhana za Kiingereza *documentary translation* na *instrumental translation*, mtawalia. Nord anasema kuwa tafsiri hifadhi hutunza elementi za LC; kwa hiyo, ni kirejeleo cha mawasiliano ya kitamaduni chanzi kati ya mwandishi na mpokeaji wa MC. Tafsiri hii huhifadhi maana asilia ya mwandishi wa MC (Gile, 2009). Ni tafsiri yenye elementi au masalia ya LC. Tafsiri hizi, kwa hiyo, humfanya msomaji wa ML ahisi kuwa anachosoma ni tafsiri, yaani kimetokana na andiko lingine. Nord anatoa mfano wa tafsiri hifadhi kuwa ni maandiko ya kifasihi, ambako ML humtaka msomaji wa MC kurejelea ujumbe wa MC. Mifano mingine inayotolewa na Nord ni tafsiri ya neno kwa neno na tafsiri sisisi/kigeni. Katika tafsiri sisisi, baadhi ya elementi za kileksika huhawilishwa kama zilivyo ili kudumisha uasilia wa MC, hasa aina za vyakula, majina ya watu, kampuni na nembo za biashara. Nord anasema kuwa urejeleaji wa MC hufanyika ikiwa tu msomaji wa matini hiyo anaelewa kuwa matini anayoisoma ni tafsiri (ML). Kwa kuwa matini yenye elementi za LC husomeka kigeni, ni dhahiri kuwa msomaji hukumbana na vikwazo vya kuelewa, ambapo hulazimika kurejea kusoma MC ya matini anayoisoma. Kwa upande mwingine, Nord anasema kuwa tafsiri wenzo hutumika kama zana huru ya kuhawilisha ujumbe katika mchakato mpya wa mawasiliano katika utamaduni lengwa. Tafsiri hii inakusudiwa kukidhi mawasiliano bila wasomaji kuhisi au kujua kama kuna matini nyingine iliyotumika katika mawasiliano mengine. Kwa maneno mengine, wapokeaji wa ML wanasoma ML kana kwamba ndio MC iliyoandikwa kwa lugha yao. Matumizi yake yanaweza kuwa yaleyale kwa matini zote. Nord anatoa mfano wa tafsiri ya mwongozo wa kompyuta au maunzi laini ambazo zinaweza kutumika kuelekeza mpokeaji wa ML kwa namna ileile ya MC. Nord anaiita tafsiri hii tafsiri zingatia-uamilifu. Kupitia ufafanuzi uliotangulia, tunaona kuwa tafsiri hifadhi inajumuisha aina kuu tatu za tafsiri ambazo ni tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi na tafsiri ya kisemantiki; na tafsiri wenzo ni ya kimawasiliano au huru.

Masalia ya LC yameendelea kuonekana katika tafsiri, hasa tafsiri za *Biblia Takatifu,* licha ya tafsiri hizi kuonekana kuwa hazizingatii maumbo, muundo, mtindo, muktadha na utamaduni wa LL hata kuwatatiza wasomaji wa ML kuelewa (Newmark, 1981; Mwansoko, Mekacha, Masoko na Mtesigwa, 2015). Kimsingi, makala hii imebainisha, imechambua na kueleza dhima ya maneno ya lugha chasili ambayo yameendelea kuwapo katika *Biblia* hadi sasa. Maswali yaliyoongoza mjadala wa makala makala hii ni mawili. Nayo ni: 1. Je, katika Biblia maneno yapi ni ya lugha chasili? 2. Kwa nini maneno hayo yaendelee kuwapo katika lugha lengwa, hasa Kiswahili? Kwa hiyo, makala hii imebainisha maneno ya Kiyunani, Kilatini na Kigiriki yaliyomo katika *Biblia Takatifu* iliyoandikwa kwa Kiswahili pamoja na kufafanua dhima ya maneno hayo.

**Dhima ya Tafsiri Hifadhi katika *Biblia Takatifu***

Uchambuzi unaonesha kuwa masalia ya lugha za awali zilizotumika kuandika *Biblia Takatifu*, hasa maneno ya Kiyunani na baadaye Kilatini (Kigiritini),[9] yana dhima mbalimbali katika ML. Miongoni mwa dhima hizo ni kutunza utukufu wa Kimungu, kutunza historia na kumbukumbu za mambo na matukio ya kitamaduni yahusuyo imani ya Kikristo na kuonesha msisitizo wa mambo ya Kimungu.

**Kutunza Utukufu wa Kimungu**

Masalia ya maneno ya Kiyunani na Kilatini (Kigiritini) katika *Bibilia Takatifu* yanaonesha utukufu mkuu wa Kiungu. Katika *Mwanzo 16:14*, mathalani, tunaona neno **Beer-lahai-roi** ambalo maana yake ni **Kisima cha Aliye hai anionaye** likionesha utukufu wa Kiungu. Kisima kile kilichoitwa **Beer-lahai-roi**, kipo kati ya Kadeshi na Beredi, ambako McNamar (2011) anasema ni eneo la Maka ya sasa. **Beer-la'hai-roi** ni kisima kilichopata jina hili baada ya BWANA (au malaika wa BWANA) kumtokea Hajiri, mjakazi wa Sarai na suria wa Ibrahimu. Akihofia chuki za Sarai, Hajiri alikimbilia jangwani Beersheba akiwa na ujauzito aliobebeshwa na Ibrahimu (*Mwanzo 16:7 - 14*). Akiwa huko jangwani, malaika alimtokea na kumpa habari za matumaini; hapo ndipo Hajiri alipomwita huyo malaika, "Wewe ni Mungu uonaye" – na ndilo jila la kisima hicho. Inaaminika **Beer-lahai-roi** ni kisima kilichoambatanishwa na uchaji; hivyo, Isaka aliifanya sehemu hiyo kuwa madhabahu (Laymon, 1971) (linganisha na *Mwanzo 24:62*; *25:11b*), na hata alihamia eneo lile (*Mwanzo 16: 7*; *24: 62*; *25: 11*). Kutokana na uchaji mtakatifu wa eneo la kisima hicho, tunaona neno **Beer-lahai-roi** linaendelea kuonekana kwenye *Biblia Takatifu* ya Kiswahili hata leo hii.

Vilevile, katika *1 Samweli 2:10*, tunaona utukufu anaopewa mtumishi wa Mungu kupitia neno **masihi** ambalo, kwa Kiebrania, maana yake ni **mtiwa mafuta** au **mwenye kuwekwa wakfu kwa kutiwa mafuta** ili awe mfalme au kuhani au nabii. Kwa Kiyunani, ni **Kristo**. Tunaona neno likisema, "Washindanao na BWANA watapondwa kabisa, toka mbinguni yeye atawapigia radi, BWANA ataihukumu miisho ya dunia, naye atampa mfalme wake nguvu, na kuitukuza pembe ya masihi wake.

Neno **Messiah** (kwa Kiebrania) lina mzizi wake **mashahh** wenye maana **kukandika kwa kimiminika kizito**; na, mara nyingi, hutafsiriwa kama **kupaka** kama linavyotumika katika *Yeremia 22:14*. Neno **mashahh** pia, limetafsiriwa kama **kuweka wakfu** katika *Kutoka 29:7*. Katika ulimwengu wa *Agano la Kale*, mafuta

---

[9] Tafsiri ya kwanza ya Biblia kutoka Kiebrania kwenda Kiyunani (Greek) inayojulikana kama 'Septuagint' ilifanyika katika kipindi cha utawala wa Ptolemy II (28 1 - 246 B.K). Tafsiri ya pili ilifanyika kutoka Kiebrania kwenda Kilatini. Tafsiri ya pili inajulikana kama Vulgate na ilifanywa, kwa kiasi kikubwa, na Mt. Jerome mwishoni mwa karne ya nne B.K.

ya mizeituni yalikuwa bidhaa adimu na ndiyo yaliyotumika kuwaweka wakfu wafalme, makuhani au manabii. Kwa tafsiri halisi, **mashahh** lina maana ya **mtu aliyemwagiwa**/k**andikwa mafuta kwa ajili ya wajibu**/**mamlaka maalum**.

Katika imani ya Kiyahudi, **Masihi** au **Kristo**, kwa Kiyunani, alikuwa ni Mfalme wa kisiasa aliyekusudiwa kutoka katika Uzao wa Daudi (*Yeremia 23:5*). Ni kiongozi (aliyetarajiwa kuwa) hodari mwenye ushawishi kwa wafuasi wake na jemedari machachari atakayewashindia Waisraeli vita na atakuwa mwamuzi wa haki (*Yeremia 33:15*), ambaye angeijua sheria ya Kiyahudi na kuzilinda Amri za Mungu (*Isaya 11:2 - 5*).

Katika Agano Jipya, neno **Masihi** ama **Kristo** linatumiwa kumaanisha Yesu Kristo ambaye Wakristo wanaamini ndiye mpakwa mafuta aliyetabiriwa katika maandiko ya Kiyahudi. Ijulikane kuwa **Yesu Kristo** ni majina mawili yanayotumiwa sambamba, yaani **Yesu** *(Iēsoûs* – Kiyunani) ambalo ni sawa na **Yoshua** *(Yēshūa* – kwa Kiebrania) lenye maana ya, "**Bwana ataokoa**" au, "**Bwana ni wokovu**"[10] na **Kristo** *(Χριστός* - Kiyunani) au **Masihi** (*Mashahh* - Kiebrania) lenye maana ya **mpakwa mafuta**. Majina haya yanapotumika kwa pamoja, yaani **Yesu Kristo**, yanalenga kumtofautisha na wapakwa mafuta wengine kama vile **Yoshua** na watawala waliokuwepo kama makuhani, wafalme na manabii - *Masihi*. Mara nyingi, kulikuwa na haja ya kutofautisha ni Yesu/Yoshua yupi – akilinganishwa na **Yesu wa Nazareti** (*Yohana 18:7*), **Yesu mwana wa Daudi** (*Yohana 6:42*), na **Yesu mwana wa Yosefu** (*Luka 4:22*). Kupitia ufafanuzi huu, tunaona kuwa si kila mtu anapewa jina **masihi**, isipokuwa watumishi wa Mungu, yaani mfalme au kuhani au nabii ambao wamepakwa mafuta na kuwekwa wakfu kwa ajili ya kazi tukufu ya Mwenyezi Mungu.

**YEHOVA** ni jina la Mungu lililotukuka sana ambalo kwa Kiebrania haliwezi kutamkwa. Inaonekana Waebrania hawakumtambua Mungu kwa jina halisi, isipokuwa kwa sifa zake kama vile 'Bwana, Baba, Mwenyezi, na Mfalme. Kwa mara ya kwanza, Mungu anajifunua kwa jina lake halisi nchini Misri (*Kutoka 3:13 - 15*). Kabla ya hapo, hojaji ya Nabii Musa inadhihirisha Waebrania hawakumtambua Mungu kwa jina lake kama inavyonukuliwa katika *Kutoka 6:3*, "Nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kama Mungu Mwenyezi, bali jina langu YEHOVA sikujulikana kwao."

Tokea wakati huo, jina la Mungu limeendelea kujulikana kwa Waebrania likiwakilishwa na herufi (konsonanti) nne za Kiebrania zilizoandikwa kutokea kulia kwenda kushoto **YHWH**, lakini jina hili halikutamkika kutokana na utukufu wake.

[10] Jina *Yoshua* pia lilikuwa *Hoshea* kabla ya kubadilishwa na Nabii Musa – (*Hesabu 13:16; 1Nyakati 7:27*).

Katika tafsiri za Kiswahili, **YHWH** limetafsiriwa kama **BWANA** kwa herufi kubwa (kwa kukosa jina). Kwa upande wa Waebrania, kwa kuwa hawakuweza kulitamka jina la Mungu, mara nyingi, walimwita kwa sifa yake **ădōnāy**, ambalo lina maana ya **BWANA**. Ili waweze kuyasoma maandiko yao; na, ilipokuwa ni lazima jina la Mungu kutamkwa, baadaye Waebrania waliunganisha majina mawili **YHWH** (Jina halisi la Mungu lisilotamkika) na irabu za **Adonai** (jina la kisifa la Mungu). Hatimaye, likapatikana jina mwambatano **YaHoVaH**; hivyo, wakapata uwezo wa kulitamka katika Ibada (Moore, 1911).

Jina **YEHOVA** limetumika mara nyingi katika *Biblia Takatifu* (*Kutoka 6: 2, 6, 7, 8*; *Zaburi 68:20*; *Isaya 49:14*; *Yeremia 16:21*). Bado katika tafsiri za Kiswahili, neno BWANA badala ya YEHOVA limetumika mara nyingi kumaanisha YHWH. Katika Kumbukumbu la *Torati 6:4*, kwa mfano, imeandikwa, "Sikiliza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja." Ilipobidi, neno BWANA kama YHWH limetafsiriwa sambamba na YEHOVA kutilia msisitizo wa utukufu na kuhusisha jina la Mungu kama halisi na lenye sifa. Katika *Habakuki 3:19*, mathalani, imeandikwa, "YEHOVA ndiye BWANA" ambapo ingeweza kutafsiriwa BWANA ndiye BWANA ama YEHOVA ndiye YOHOVA. Wakati wote, maneno haya yameandikwa kwa herufi kubwa kutokana na utukufu wake pia kumtofautisha BWANA (Mungu) na Bwana (Yesu) au mabwana wengine. Yesu anathibitisha utukufu huu wa jina la Mungu pale anapoomba Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe … (*Mathayo 6:9*). Aidha, katika *Yohana 12:28*, imeandikwa, "Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, nimelitukuza, nami nitalitukuza tena." Neno tukuza, katika Kiingereza, ni '**glorify'** au **reveal the majesty.** Kwa Kiyunani, ni **ἁγιασθήτω** (*hajiasthesō)* ambapo kitenzi ἁγιάζω (*hajiazō)* humaanisha **takasa** (fanya kuwa takatifu au weka wakfu). Kwa hiyo, katika *Biblia Takatifu*, neno JEVOHA lionaonesha jina la Mungu ni tukufu na haliwezi kulinganishwa na chochote ndiyo maana mwimba Zaburi anasema, "Wajue kuwa Wewe, uitwaye jina lako YEHOVA, ndiwe peke yako Uliye juu, juu ya nchi yote (*Zaburi 83:18*)."

**Kutunza Historia na Kumbukumbu za Mambo na Matukio ya Kitamaduni**

Kupitia maandiko matakatifu, tunaona masalia ya LC yanaonesha historia na kumbukumbu ya mambo mbalimbali ya kitamaduni katika imani ya Kikristo.

Neno **Edomu** ambalo tunalipata katika *Mwanzo 25:30*, kwa mfano, linadhihirisha historia ya wekundu wa ngozi ya Adamu (mwanadamu) kupitia kwa Esau. **Edomu** maana yake ni **mwekundu**. Katika *Mwanzo 25:30*, neno linasomeka, "Esau akamwambia Yakobo, Tafadhali unipe hicho chakula chekundu nile, kwa kuwa ninazimia mimi. Kwa hiyo, walimwita jina lake **Edomu**."

**Edomu** ni Jina la Kiebrania alilotaniwa Esau (lakhabu) baada ya kujipotezea uzaliwa wake wa kwanza kwa Yakobo kwa kushawishiwa na mchemsho mwekundu (soup/stew - *nazid*). Kwa hiyo, **Edomu** maana yake ni **-ekundu**. Mzizi wake ni אדם (**dm**) ambao umetumika kuelezea 'wekundu' wa vitu kama vile ngozi, makovu, mvinyo, au dhambi (*Maombolezo 4:7*, *Mambo ya Walawi 13:42*, *Mithali 23:31* na *Isaya 1:18*). **'-ekundu'** ni rangi ambayo, mara nyingi, hutumiwa kuhusianishwa na 'damu' katika Biblia. Kupitia mzizi huu, ndipo tunapata jina **Adamu** lenye maana inayofanana, yaani *"***mtu mwenye ngozi nyekundu**", au "**-a mavumbi**/**nchi**/**ardhi**." Maneno mengine yanayotokana na mzizi huo ni אדם (**adom** - nomino, **adem** - kivumishi ama kitenzi, yote yenye maana ileile ya **'-ekundu** (*Maombolezo 4:7*; *Isaya 1:18*) au אדם (**edom**) – ambayo ni aina ya chakula alichokula Esau hata kuibua jina lake (*Mwanzo 25:25, 30*).

Inasadikiwa asili ya **Edom** (**-ekundu**) ni rangi ya ardhi au udongo wa eneo. Ni jina linalosadikiwa kuwapo kabla ya kisa cha Esau na linanukuliwa katika nakala za '*The Tell El-Amarna Tablets*' (Brit. Mus. No. 64) katika majibizano ya Utawala wa 12 wa Misri, ambako **Udumu** au **Edom** inatajwa (kwa lugha ya Kiasiria) kama **mji** au **nchi** (soma pia *Mwanzo 36:32*). Katika kitabu cha *2 Samweli 6:10*, **Edomu** linatajwa sambamba na jina la mtumishi (**Obed-edom - mtumishi wa Edom**). Baadaye, uzao wake ulijulikana kama **Waedomu** (*Mwanzo 36:43*) ambayo linamhusisha Esau kama baba wa **Waedomu** (*Mwanzo 36:9*). Hata hivyo, inaelekea ama Esau alipewa jina hili kwa kuwa rangi ya ngozi yake ilikuwa nyekundu au kwa sababu ya chakula kilichokuwa na rangi nyekundu alichokula hata kuuza uzaliwa wake wa kwanza.

Aidha, katika *Mwanzo 35:8*, tunakutana na neno jingine linaloonesha kumbukumbu **Alon-bakuthi** lenye maana ya **mwaloni wa vilio**. Imeandikwa, "Akafa Debora mlezi wa Rebeka, akazikwa chini ya Betheli, chini ya mwaloni; na jina lake likaitwa **Alon-bakuthi**." Wakati neno **mwaloni** lina maana ya **mti**, **bakuthi** lina maana ya **vilio**. Tukiachilia mbali simulizi za historia ya etimolojia ya maneno haya, hatuna habari za kutosha za kwa nini tangazo hili la msiba wa Debora au aya hii imechomekwa katikati ya vifungu hivi. Maelezo yaliyotangulia na yanayoendelea hayashabihiani na kifungu hiki. Kwa mara ya kwanza kabisa, jina 'Debora,'[11] ndio linatajwa wazi katika kifungu hiki, huku likiwa limejitokeza ghafla na kuingilia mtiririko wa masimulizi yaliyotangulia na yanayoendelea. Katika *Mwanzo 24:59*, Debora ametambulishwa kwa jina la 'Yaya' wa Rebeka bila kutajwa jina. Kwa hiyo, alikuwa ni yaya na inasadikika alikuwa ni yaya-mnyonyeshaji (na, kwa hiyo, yeye ndiye aliyemnyonyeshea na kumkuzia Rebeka watoto wake—Yakobo na Esau). Baadaye, inaonekana alikuwa ni mshauri wa nyumba ya Yakobo.

[11] Debora huyu ni tofauti na yule Mwamuzi.

Mwanatheolojia Martin Luther, anamtaja Debora kama "mwanamke mwenye hekima na mlezi wa Kimungu ambaye utumishi na ushauri wake ulitumika kuendesha nyumba ya Yakobo.

Kulikuwa na utamaduni, hasa kwa familia za hadhi ya juu, kuajiri mayaya wa kunyonyesha watoto wao (linganisha *Kutoka 2:7*; *2 Wafalme 11:2*). Kwa kawaida, yaya wa namna hii alikuwa na wajibu, sio tu wa kumyonyesha mtoto, bali kumlea na kumkuza katika kusudi tarajiwa[12].

Suala la mazishi kufanyika chini ya mti, halikuwa la ajabu, isipokuwa kisicho cha kawaida katika kifungu hiki ni nafasi ya Debora katika familia hii hata kupewa heshima ya mazishi makubwa na maombolezo makubwa (ya mtu muhimu katika Israeli). Wachambuzi wa Biblia wanaamini kuwa mazishi yake yametajwa kwa makusudi sambamba na vifo na mazishi ya watu wengine maarufu (Abrahamu, *Mwanzo 25:7 - 11*; Isaka, *Mwanzo 35:29*; Yakobo, *Mwanzo 49:33*). Kabla ya kutangazwa kwa msiba wa Debora, ni misiba michache—tena ya wanawake maarufu tu—ndio imetangulia (Sarai, *Mwanzo 23:1 - 20*; Raheli, *Mwanzo 35:19*). Wanatheolojia wanadhani Debora alipewa hadhi kubwa hata kupita ile ya Rebeka aliyemlea na ambaye msiba wake unatajwa bila uzito mkubwa (*Mwanzo 49:31*).

Kwa kawaida, watu wenye heshima au umaarufu katika Israeli walihifadhiwa kipekee kwa ajili ya kumbukumbu za vizazi vya baadaye na uchaji (*Mwanzo 47:*29 - 30; *49:29 - 32*; *50:25*; *Kutoka 13:19*). Kuzikwa kwa Debora mahali hapa ni ishara ya wazi kuwa mahali pake sio tu palikusudiwa kuwa na heshima ya kimadhabahu, bali, pia, kwa kuwa Yakobo alishajitwalia eneo hilo kama sehemu ya ahadi ya Mungu ya kumiliki nchi. Inaonekana Yakobo alitaka Debora awe ni sehemu ya ahadi hiyo na, labda, vizazi vya baadaye vienzi kaburi lake. Kwa hiyo, neno **Alon-bakuthi** linatukumbusha kuwa waliozikwa pahala pale walikuwa watu maarufu na walioheshimika katika jamii akiwamo Debora.

Neno lingine lililotunza kumbukumbu katika *Biblia Takatifu* ni **pasaka**. Ingawa katika dini ya Kikristo neno **pasaka** linahusishwa na kifo cha Bwana Yesu, kimsingi hata Yesu mwenyewe pamoja na wazazi wake waliadhimisha pasaka

[12] Chambuzi kadhaa zinamtaja Debora kuwa 'Mkunga' wa Rabeka, hivyo, alihusika katika kuzaliwa kwa Esau na Yakobo; na, pengine, alielewa ahadi zilizoambatana na kuzaliwa kwao. Hivyo, alikuwa sehemu ya kutunza siri hiyo ya Mungu na kuitimiza katika uzao huo (Martin Luther, 1970). Luther anaongeza kuwa Debora amedumu katika ukunga kwa miaka karibia 130 toka Rebeka na Isaka walipooana na baadaye Esau na Yakobo kuzaliwa. Kwa mujibu wa Luther, Deborah amemkuza na kuendelea kuishi na Yakobo. Alipokufa, umri wake ulikuwa karibia miaka 186 hivi. Alichukuliwa kama "bibi" aliyejaa mafundisho (*doctrine*) na "uzoefu katika masuala mengi. Aidha, alichukuliwa kama mtu aliyestahili heshima ya hali ya juu (*reverence*) ya familia na jamii ya Kanisa kwa ujumla."

(*Mathayo 26:17*; *Yohana 12:1*; *Luka 2:41 - 42*). Tukio la kusulubishwa kwa Yesu sio chanzo cha pasaka, bali lilifanyika wakati wa Pasaka.

Asili ya **pasaka** ni **Pesach** (kwa Kiebrania). Ni neno ambalo linatafsiriwa kama '*Passover'* kwa Kiingereza, yaani 'kupita juu ya'. Hii ni siku ya Kiyahudi ya kukumbuka wakati ambapo Mungu alipita juu ya nyumba za wana wa Israeli akiwaua wazawa wote wa kwanza wa Wamisri katika pigo lile la kumi (na la mwisho) lililomlazimisha Mfalme Farao kuwaachilia huru kutoka utumwani Misri. Hakuna kumbukumbu za kihistoria juu ya tukio hili la ukombozi au utumwa wa Waisraeli kule Misri. Hata hivyo, katika kalenda ya Kiyahudi, limenukuliwa kutokea siku moja kabla ya sikukuu ya Kiyahudi ya mazao iliyojulikana kama **Mikate isiyotiwa chachu** iliyoadhimishwa kwa sadaka za kumshukuru Mungu kwa mazao ya awali. Tangazo la pasaka lilianza usiku wa tarehe ya 14 ya mwezi wa Kwanza wa Kiyahudi – Nisan (*Mambo ya Walawi 23:5*). Mwezi huu, kwenye Torati, unajulikana pia kama Abibu (*Kumbukumbu la Torati 16:1*) sawa na Aprili kwa kalenda ya Gregori.

Kupitia Nabii Musa, Mungu anawaagiza Wayahudi kumchinja mzaliwa wa Kwanza wa mwanakondoo asiye na waa (*Kutoka 12:6 - 20*; *1:4*; *Kumbukumbu la Torati 16:1*), na kupaka damu yake katika miimo ya nyumba zao kama alama ambayo ingetofautisha nyumba zao na za Wamisri pale Mungu alipopita kuwaua wazaliwa wa kwanza (*Mambo ya Walawi 23:5 - 6*; *23:10 - 16*). Baada ya **Pasach**, ndipo 'kutoka' kwa Wayahudi huko Misri kulipoasisiwa. Kwa kifupi, utamaduni wa pasaka ni kuwakumbusha Wayahudi kwamba, kupitia damu ya mwanakondoo, Mungu aliwakomboa kutoka Misri. Walipaswa kudumisha utamaduni huo kwa kusimuliana na kutoa sadaka. Wakaadhimisha katika nchi ya Sinai, kwa mara ya kwanza, wakiwa huru (*Hesabu 9:5*), na mara ya pili Gilgali wakiikabili nchi ya ahadi (*Joshua 5:10 - 11*) na wakaendeleza utamaduni huo hata walipokuwa uhamishoni (*Ezra 6: 19 - 22*).

Baadaye, maana ya **pasaka** inachukua tafsiri mpya katika Agano Jipya, ambapo kifo cha Yesu Kristo kinabeba mbadala wa mwanakondoo wa pasaka kama Mtume Paulo anavyobainisha (*1 Wakorinto 5:7 - 8*). Ingawa Wayahudi wameendelea kudumisha pasaka ya asili, miaka kadhaa baada ya Kristo, Wakristo waliidhimisha siku hii kwamba Mungu, kupitia damu ya Yesu Kristo, aliukomboa ulimwengu kutoka katika utumwa wa dhambi (*1 Wakorinto 11:17 - 34*).

**Kuonesha Msisitizo**

Uchambuzi wa vifungu katika *Biblia Takatifu* unaonesha kuwa masalia katika tafsiri yanasisitiza mambo mbalimbali. Tunaona neno **yubile** katika *Mambo ya Walawi 25:10* likisisitiza mambo muhimu ya Kimungu. Yubile, kwa asili, maana

yake ni **Baragumu lililopigwa kila mwaka wa hamsini**. Imeandikwa, "Na mwaka wa hamsini nitautakasa, na kuwatangazia uhuru watu wote katika nchi; itakuwa ni mwaka wa yubile. Nanyi kila mtu atairudia milki yake mwenyewe, nanyi mtarejea kila mtu kwa jamii yake." TUKI (2014) inafasili neno **Jubilei**/**Jubilii** (kisawe cha **yubile**) kama "sehemu katika maisha ya watu, shirika, asasi, n.k. ambayo hufanywa kila baada ya kipindi fulani kama vile miaka 25, 50, 75 au 100, mathalani, tangu kufunga ndoa au kuanzishwa shirika." Kimsingi, **yubile** ni neno lililotoholewa kutoka neno la Kiebrania יבל (**yabal**) au **Mwaka wa Yubile** (שנת היובל) (*Mambo ya Walawi 25:13 - 54*; *27:17 - 24*; *Hesabu 36:4*).

Kitenzi cha Kiebrania יבל(**yabal**) kina maana ya **kutoa**/**kuzalisha**. Kutokana na kitenzi hicho, linapatikana jina (la jinsia ya kiume) – יובל (**yobel**) linaloweza kutafsiriwa kama 'mtoaji' au 'upembe wa mwanakondoo' (*Kutoka 19:13*; *Joshua 6:5*; linganisha pia na *Mambo ya Walawi 25:13l* na *Hesabu 36:4*) kwa sababu Baragumu ilipigwa kwa kutumia upembe wa kondoo kuashiria mwanzo wa **yubile** (*Mambo ya Walawi 25:9*). Katika kitabu cha *Ezekieli 46:17*, nabii anautaja kama mwaka wa kuacha huru.

Katika utamaduni wa Kiyahudi, Mwaka wa Sabato ulisherehekewa kila baada ya miaka saba; na kila Sabato saba, Sabato kubwa au **yubile** ilisherehekewa. Kwa mujibu wa *Mambo ya Walawi 25:8 - 55*, kulikuwa na misingi ifuatayo ya yubile:

1. Kama ilivyokuwa katika Mwaka wa Sabato (*Mambo ya Walawi 25:2 - 7*) ardhi ilipaswa kupumzishwa. Watu hawakuruhusiwa kuilima ardhi (ili ijikusanyie rutuba), bali kula vyakula vilivyojiotea kwa asili. Hivyo, huu ulikuwa ni mwaka wa mapumziko sio tu kwa watu bali pia kwa ardhi;
2. Ni mwaka ambao watumwa waliachiwa huru na wadeni kusamehewa madeni yao. Katika utamaduni wa Kiyahudi, watu masikini waliruhusiwa kutumika kwa wenye uwezo kama watumwa kwa miaka kadhaa ili kulipa madeni yao. Ingawa wamiliki walipaswa kuwahudumia watumwa kwa ukarimu kuhakikisha kuwa hakuna mtumwa au masikini atakayebaki kuwa mtumwa maisha yote au kudhibiti madeni yasiyolipika, ilikuwa ni lazima kuwaachia huru watumwa wote katika mwaka wa yubile ili kuanza upya mzunguko wa kibiashara; na
3. Ardhi yote iliyomilikiwa kwa muda au kununuliwa ilipaswa kurudishwa kwa mmiliki wake halisi (wa awali). Kimsingi, mtu aliyeuza ardhi hakuwa ameuza ardhi, bali mazao ya ardhi na, hivyo, bei ya manunuzi pia ilitegemeana na kipindi kabla ya yubile kwani ardhi ingerudi kwa mwenyewe tena. Hili lilifanyika ili kuhakikisha kuwa hakuna tajiri aliyejilimbikizia mali za watu wengine; na, kwamba, hakuna masikini atakayebaki kuwa masikini milele ama kushindwa kulipa madeni yake.

Kitheolojia, neno yubile linabeba maana kuu mbili: i) Kwamba ardhi ni ya Bwana; hivyo, watu wamedhaminiwa kuilima na sio kujibinafsishia (*Isaya 5:8*); na, ii) kwamba ni kusudi la Mungu kwamba watu wake wote wawe huru.

Kupitia mjadala huu, kwa hiyo, tunaona kuwa kuendelea kutumia neno **yubile** katika *Biblia Takatifu* kunasisitiza kuwa ardhi ni mali ya Mungu; hivyo, isitumike kinyume na makusudi ya Mungu na kusisitiza uhuru wa watu wa Mungu, hasa kiroho. Mwaka wa Yubile ni wa matengenezo ya kiroho kwa watu wa Mungu.

Neno **Amin - Amen** ni moja ya maneno maarufu katika *Biblia* na desturi za kiibada. *Kamusi ya Kiswahili* (2014), inalitafsiri neno **amin!** kama, "kiitikio cha dua au sala: na iwe hivyo". Pamoja na hivyo, kuna tofauti katika *Biblia*, ambapo neno **Amin!** limetumika mara nyingi katikati ya sentensi tofauti na **amin**(**a**) ilivyotumika mara nyingi mwishoni mwa sala (*Mathayo 6:9 - 13*).

Neno 'amin - amina' ni masalia ya neno la Kiebrania na Kilatini **amen** ambalo limetumika zaidi ya mara elfu katika *Biblia Takatifu*. Tafsiri yake sio rahisi; haipatikani kirahisi, bali inategemeana na mahali neno lilipotumika. Kwa Kiswahili, **amin** ni baadhi ya maneno nadra yanayoishia pasipo irabu.

Katika Biblia, kwa mara ya kwanza, 'amina' linajitokeza katika kitabu cha *Hesabu 5:12 - 31* wakati mwanamke aliyesingiziwa ugoni na mumewe akiwasilishwa mbele za uwepo wa Mungu kula kiapo cha uaminifu. Wakati wa kiapo kilichoambatana na kuhani kutoa laana, mwanamke anatakiwa kuitika "Amina, Amina" (*Hesabu 5:22*). Hapa neno 'amina' linatumika kwa mara ya kwanza kama sheria ya kujitetea kutokuwa na hatia mbele za BWANA. Katika matumizi haya, linaonekana kumaanisha **hakika isiyotilia mashaka**, **ndio naamini hivyo**, **ni ukweli mtupu utokao moyoni** au **naamini yote niliyosema kwa hakika**. Ni katika mazingira haya ambapo, kwa Wayahudi, kila baada ya maombi, unabii kutolewa au sheria kusomwa, watu wote waliitikia 'Amina' (*Nehemia 5:13; 8:6*), yaani ni hakika au na iwe hivyo.

Katika matumizi mengine, neno hili limetumika kama jina la Mungu. Katika *Ufunuo 3:14*, BWANA Mungu anajulikana kama **Amina**, yaani **shahidi mwaminifu na wa kweli**." Katika *Isaya 65:16*, pia anaitwa **Mungu wa kweli**, ambapo inaweza pia kutafsiriwa kama **Mungu wa Amina**.

Mara kadhaa **amin**'limesisitizwa. *Nehemia 8:6* anatumia **Amen**, **Amen**, kusisitiza imani isiyo na mashaka kwa Mungu, na *Zaburi 89:52* **Amina** na **Amina** kama sehemu ya baraka za mwisho wa ibada kwa BWANA (Laymon, 1971). *Yeremia 28:6* anapolitumia mara mbili, anamaanisha '**Amina**, yaani BWANA na atende hivi.' Maneno **atende hivi** ni sawasawa na 'amina.' Kwa hiyo, hapa ni sawa na kusema "amina amina." Yeremia anasisitiza mamlaka na hakika ya Mungu wa Wayahudi akimtofautisha na miungu ya kipagani (Laymon, *katajwa*).

Katika Agano Jipya, Yesu Kristo amenukuliwa mara nyingi akitumia maneno **ἀμήν λέγωύ μίν** – (**amen lego humin - kweli kweli nakuambia**) (*Yohana 3:3*, *5*; angalia pia *Mathayo 6:2, 5, 16*; *18:3*; *Luka 13:35*; *Yohana 5:19*, *24*, *25*; *6:26*, *32*, *47*, *53*). Inaonekana katika mazingira haya Yesu alikusudia sio tu kuwaaminisha wasikilizaji wake juu ya ukweli wa maneno yake, bali pia alipenyeza nafasi ya uungu wake au ushirika wake na Mungu. Ilikuwa ni namna ya Yesu kusema maneno yake ni hakika isiyoacha shaka, tofauti na maneno yoyote waliyowahi kuyasikia (Kittel & Friedrich, 1985). Kwa mfano, katika hotuba yake, Mathayo anatumia maneno 'mmesikia …' 'imenenwa …' na kuhitimisha na neno 'amin' (*Mathayo 5:26*) kuonesha kuwa mamlaka yake ni ya kipekee na inazidi ile ya wasomi wa Kiyahudi. Kwa maneno mengine, kwa kutumia neno **amina**, ni kama Yesu anasema yeye ana uungu; na, kwa hiyo, maneno yake ni 'kweli' tupu.

Mtume Paulo analitumia neno **Amin** kama kiapo/uthibitisho anaposema, "Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amina … (*2 Wakorinto 1:20*).

Vilevile, mazingira ya *Luka 9:27* yanaonesha neno **Αληθος (alethos**) alilolitumia lina maana ya 'kweli' ingawa amelitofautisha na **ἀμὴν** (**amen**) kama lilivyotafsiriwa katika *Marko 9:1* na kwingineko. Katika tafsiri za Kiingereza, maneno hayo mawili, **Αληθος** na **ἀμὴν** yametafsiriwa kama **truth** au **verity**, lakini kwa Kiswahili, mara kadhaa, neno **amin** limeachwa lilivyo, wakati neno **alethos** limetafsiriwa kama 'kweli' (*Luka 9:27*).

Katika ujumla wake, **amen** limetumiwa katika mazingira makuu matatu; kukubaliana na matakwa ya Mungu yanayotegemea mapenzi yake, kuthibitisha nguvu za Mungu: laana au vitisho (*Hesabu 5:22*), na kukiri sifa za Mungu kama sehemu ya ibada.

## Hitimisho

Makala hii imechambua dhima ya tafsiri hifadhi kwa kujielekeza katika *Biblia: Maandiko Matakatifu*. Uchambuzi unaonesha kuwa tafsiri hiyo ina dhima kubwa sana katika andiko hilo. Masalia ya maneno ya Kiyunani na Kilatini, mathalani, pamoja na dhima nyingine, yanatunza utukufu wa Kimungu, historia na kumbukumbu ya mambo ya kitamaduni na kuonesha msisitizo wa mambo ya Kimungu. Makala hii inapendekeza kwamba wasomaji wa tafsiri hifadhi wasiichukulie tafsiri hii kwa wepesi kwa sababu inaatamia maudhui mazito. Hivyo, wasomapo, wajijuvye vya kutosha kuhusu masalia ya lugha chanzi yaliyomo katika matini lengwa husika ili waweze kuelewa ujumbe uliomo katika matini kikamilifu. Wasomaji hawa wanaweza kujijuvya dhima za masalio hayo kupitia kamusi, kusoma maandiko chanzi mengine na kuwakabili wazungumzaji wa lugha chanzi.

**Marejeleo**

Gile, D. (2009). *Basic Concepts and Models for Interpreter and Translator Training.* Amsterdam: John Benjamins Publishing.

Kittel, G. na Friedrich, G. (wah.) (1985). *Theological Dictionary of the New Testament.* Abridged in one Volume by Geoggrey W. Bromiley. Michigan: William B. Eermans Publishing Company.

Laymon, C. (mh.) (1971). *The Interpreter's One-Volume Commentary of the Bible.* New York: Abingdon Press.

Laymon, C. (1971). The Interpreter's Onve-Volume Commentary on the Bible: Introduction and Commentary for Each Book of the Bible Including the Apocrypha, with General Articles. N.York: Abingdon Press.

McNamar, M. (2011). *Targum and New Testament: Collected Essays,* Tübingen: Mohr Siebeck.

Moore, G. (1911). "Jehovah" katika *Encyclopaedia Britannica* Juzuu 15, Toleo 11.

Mpemba, T. (2016). Nadharia za Tafsiri na Ukalimani. Katika Jilala, H. (mh.), *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*, 2 - 18). Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited.

Munday, J. (2008). *Introducing Translation Studies*. *Theories and Applications, Toleo la Pili*, London: Routledge.

Mwansoko, H.J.M., Mekacha, R., Masoko, D., & Mtesigwa, P. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu, Toleo la Nne.* Dar es Salaam: TATAKI.

Newmark, P. (1981). *Approaches to Translation*. Oxford: Pergamon Press.

Nord, C. (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology, and Didactic Application of a Model for Translation-oriented Text Analysis*. Amsterdam: Rodopi.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 3*. Nairobi: Oxford University Press.

Vyama vya Biblia vya Kenya na Tanzania (1997). *Biblia: Maandiko Matakatifu*. Vyama vya Biblia vya Kenya na Tanzania: Nairobi na Dodoma.